

## Disemba 2016

“Maana kwa ajili yetu amezaliwa, Tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa mabegani mwake.Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani.” Isaya 9:6

Wapendwa waombaji,



Ni furaha ilioje kusherehekea pamoja na nyinyi kuzaliwa kwa Mwokozi Yesu Kristo. Tunapoanza maombi yetu ya mwezi Disemba, nakuomba ukumbuke kuombea familia na marafiki ambao hawajamjua Yesu kama Mwokozi wao.

Najua kuwa mara zingine tunapoangalia mambo yanayoendelea ulimwenguni, tunaweza kukosa matumaini ya kuwa mambo yatabadilika. Tunaweza kujaribiwa kukata tamaa au kupoteza matumaini kuwa Mungu anayesikia maombi yetu. Hata hivyo, ninaamini kuwa maombi yenye uaminifu ndio majibu ya kutokukata tamaa. Kwa imani, tunaamini kuwa yupo Mungu anayesikia na yupo karibu na wale waliovunjika mioyo. Kwa imani, tunaamini kuwa tunapokutanika kuomba, Mungu anakuweupo.

Wanawake tunaoomba tunaamini kuwa maombi yetu yanaweza kujibiwa hata tunapokuwa hatuoni majibu kwa macho haya ya mwili. Tunafahamu kuwa tunapokuwa hatujui kitu cha kufanya, tunamuomba Mungu anayejua kila kitu na anayefanya kila kitu ili kutimiza kusudi lake. Tunapokutana na vikwazo tena na tena, tunaomba, tukiamini kuwa tunayaweza mambo yote katika Kristo atutiaye nguvu. Hatutakiwi kukata tamaa ndani ya Kristo ambaye upendo wake ni ule ule jana, leo na hata milele.

Asante sana kwa mwaka mzuri wa maombi. Muda wako wa kujitoa usioweza kuhesabika uliugusa moyo wangu kwa ndani sana. Ninautazamia mwaka mwingine tena wa mahitaji ya maombi ambao tutavamia milango ya mbinguni sauti zitakapoliihua Jina la Yesu ulimwenguni. Asante kwa kuamini na kuomba kwa Mungu ambaye yupo karibu sana na anayesikia vilio vyatubu zake.

Na asante kwa upendo na msaada wako ambao ni endelevu, nikiamini kuwa yupo Mungu anayeweza kuyafanya mengi, zaidi ya yale tuyawazayo (Waefeso 3:20). Tafadhali endelea kuombea uongozi wa Mungu na muelekeo tunapoingia katika mwaka mwingine wa utumishi wenye uaminifu kwa Mungu wetu, tukimuomba Mungu awalete watu wengi zaidi, na waombaji wengi zaidi waungane nasi katika mwaka huu unaoanza.

Katika yeye Miyo yetu inashangilia,

Peggy Banks  
Mkurugenzi wa Huduma kimataifa  
Project Hannah